

Elimu bora ya mifugo yatakiwa kuimarishwa ndani na nje ya nchi

■ Na Betty Mrema,
Dar es Salaam

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Tixon Nzunda, ametaka Wakala ya Elimu ya Mafunzo ya Mifugo nchini (LITA) kuhakikisha iratoa elimu bora ya mifugo ndani na nje ya nchi.

Nzunda aliyasema hayo juzi jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha tisa cha Baraza Kuu

la Wafanyakazi la LITA na kuwataka kuwa chanzo cha kuwashauri wafugaji na kutoa maarifa kwa wadau wa sekta ya mifugo ili iweze kuimarika na kuwa ya kisasa zaidi.

Alisema wakufunzi wa LITA wanatakiwa kuwa chanzo cha kuandaa majarida mbalimbali vikiwamo vitabu vya ufugaji na kupatikana kwa maarifa mapya yanayotokana na tafiti zinazofanywa na wakufunzi hao.

Aidha, alisema wajibu wa LITA ni kuwa karibu na umma kwa kutoa huduma bora ikiwamo ya wanafunzi wanaohitimu

kuwa bora na wanaoheshimika, kutambulika, wenye maarifa, wanajiamini na kuandaliwa vizuri kwenda kusaidia sekta binafsi.

Awali Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi la LITA, Dkt. Pius Mwambene, alisema imeendelea kumarisha uhusiano na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha inaboresha miundombinu ya kufundishia.

Alisema kwa sasa wakala huo unakaribu kukamilisha makubaliano ya ujeruzi wa kampasi ya Lita Mkoani Songwe ikiwa ni jitahada za kuongeza wigo wa elimu ya mifugo katika

maeneo mbalimbali nchini.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Angello Mwilawa, alisema wataendelea kusimamia maadili na weledi kwa wafanyakazi na kuongeza ushirikishwaji ili kuwepo na matokeo makubwa yenye maslahi mapana yatakayoleta tija.

Dkt. Mwilawa alisema nguvu zaidi zitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yatagusa jamii na maelekezo yote yatafanywa kazi ili kuongeza ufinisi.

DAILY NEWS, MARCH 30, 2022 Pg 2

AU member states urged to enhance sustainable fishing

By DAILY NEWS
Reporter

LIVESTOCK and Fisheries Deputy Minister Abdallah Ulega has called on the African Union member states to continue enhancing sustainable fishing since the sector plays an important socio-economic role in building national economies.

He said the economies are built through income generation, employment and food security thus supporting multitude of livelihoods.

Mr Ulega made the remarks in Dar es Salaam yesterday when officiating a consultative meeting which involved the AU member states.

"We are all aware that there is an ever-increasing demand for fish and fisheries products over the past decade. Trade in fish and fishery products now constitute the most highly traded food commodities internationally, leading to increase in demand which have some negative impacts on the fishing ecosystems and environment as well as declining fish stocks," he said.

He said African countries were facing common challenges in fisheries management such as overfished stocks, illegal, unreported and unregulated (IUU) fishing, inadequate benefits from trade in fish and fish products therefore they need to be careful on how

to meet increasing fish demand and promote sustainable fisheries industry in Africa.

According to him, the implementation of the Policy Framework and Reform Strategy for Fisheries and Aquaculture in Africa and the African Fisheries Reform Mechanism will go a long way in helping AU member states to address some of those challenges and bring the sector to the reform path.

"Tanzania is committed to the conservation of our fisheries resources and sustainable development of aquaculture. My Ministry is working closely with the key players in the fisheries sector, including fishers, aqua farmers, fish processors and exporters, regional fisheries management bodies, relevant regional multilateral environment agreements, the private sector and the development partners to bring about reforms and improved governance of the fisheries sector with a view to increasing socio-economic benefits and stock sustainability", he added.

He further congratulated the African Union for spearheading the development of the Policy Framework and Reform Strategy for Fisheries and Aquaculture in Africa (PFRS) as well as the African Fisheries Reform Mechanism (AFRM) and their proactive leadership in the implementation of the Fisheries Governance Projects

(FISHGOV) in Africa.

He noted that the PFRS and the AFRM through the FISHGOV projects have provided the much needed guidance to the African Union Member States in the actualization of the Malabo Declaration on Accelerated Agricultural Growth and Transformation for Shared Prosperity and Improved Livelihoods.

The Director of AU-IBAR, Dr Nick Nwankpa said that the overall purpose of the meeting was in line with the activities as provided for by the FishGov 2 project.

He encouraged the participants to analyse the possibility for the programme to focus at key issues affecting all African countries and particularly prioritise a strategy to increase the rate of adoption, domestication and implementation of those Global Instruments as a gateway to tackle key challenges and constraints affecting the growth of the fisheries and aquaculture sector.

"Our attention should be on enhancing partnerships, participation in high seas fisheries, market access and integration, equitable investments, sustainable fisheries and resources exploitation and illegal fishing which result in depletion of the fisheries resources and loss of income amounting to billions of dollars for the continent", Dr Nwankpa elaborated

AGIZO>>Elimu inayotolewa iwe ya manufaa kwa sekt

Dk. Nzunda aagiza elimu bora ya mifugo

Na MWANDISHI WETU

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Tixon Nzunda, ameutaka Wakala ya Elimu ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kuwa chanzo cha elimu bora ya mifugo nchini.

Nzunda alisema hayo juzi wakati akifungua rasmi kikao cha tisa cha Baraza Kuu la Wafanyakazi wa LITA na kubainisha kuwa ni wakati sasa wakala huo kuwa chanzo cha kuwashauri wafugaji na kutoa maarifa kwa wadau ili sekta hiyo iwe ya kisasa.

Aliongeza kuwa, wakufunzi wa LITA wanatakiwa pia kuwa chanzo cha kuandaa majarida mbalimbali vikiwemo vitabu vya ufugaji na kuwa chanzo cha kubuni na kupatikana kwa maarifa mapya yanayotokana na utafiti unazofanywa na wakufunzi

hao.

Katibu mkuu huyo alifafanua kuwa, wajibu wa LITA ni kuwa karibu na umma kwa kutoa huduma bora ikiwemo ya wanafunzi wanaohitimu kuwa bora na wanaoheshimika, kutambulika, wenye maarifa, wanaojiamini na kuandaliwa vizuri kwenda kusaidia sekta binafsi.

Awali Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi la LITA, Dk. Pius Mwambene, akizungumza kabla ya ufunguzi rasmi wa kikao hicho, alisema wakala huo umeendelea kuimarisha uhusiano na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuboresha miundombinu ya kufundishia.

Dk. Mwambene ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa LITA, alifafanua kuwa kwa sasa wakala huo unakaribia kukamilisha makubaliano ya ujenzi wa kampasi yake mkoani Songwe

zikiwa jitahada za kuongeza wigo wa elimu ya mifugo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aliongeza kuwa, katika kuhakikisha wafugaji wanapata mwongozo wa ufugaji bora imeainisha utaratibu wa kuwashikiza wanafunzi wa hatua ya nne kwa wafugaji katika maeneo yao wakati wa likizo ili kuanza kujenga uzoefu ujasiri wa kuwahudumia wafugaji mapema.

Pia, amebainisha kuhusu vikao vya Baraza Kuu la Wafanyakazi LITA, kuwa vinalenga kuushauri wakala kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa katika sheria, kupokea na kujadili makadirio ya mapato kwenye matumizi ya wakala na kujadili mipango ya utekelezaji wake kwa ajili ya ustawi wa wakala na wafanyakazi wake.

Kutokana na malengo hayo amewataka wajumbe wa baraza kushiriki kikamilifu na kutoa maoni na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya wakala.

Akitoa neno la shukrani, Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dk. Angello Mwilawa alisema wataendelea kusimamia maadili na weledi kwa wafanyakazi na kuongeza ushirikishwaji ili kuwa na matokeo makubwa yenye maslahi manana vatakapoleta tiia.

RI ZA DODOMA

HABARI LEO UK 5.

Nzunda ataka vyuo vya Lita kuwa kitovu cha ushindani

Na Mwandishi Wetu

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda ameuagiza Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kufanya mageuzi na kuwa kitovu cha mafunzo na ushindani katika sekta ya mifugo ndani na nje ya Tanzania.

Nzunda ameyasema hayo jana jijini hapa wakati wa kufungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi la LITA.

Alisema ni vyema kuacha kufanya kazi kimazoea na kufanya mageuzi yatakayoifanya LITA kuwa kitovu cha mafunzo katika sekta ya mifugo na kuwa na ushindani katika ngazi ya kimataifa.

"Kila siku lazima ujipime kwa matokeo yanayopimika, kwa kuangalia umechangia nini katika maendeleo na kuiletea

heshima LITA ndani ya siku au wiki au mwezi kwa matokeo ya yanayopimika."

"Nategemea muwe kitovu cha elimu ndani na nje ya nchi na Afrika Mashariki na Kati na ushindani katika ngazi za kimataifa," alisema.

Nzunda pia aliwataka wakufunzi hao kuwa wabunifu na kutoa maarifa mapya katika sekta ya ufugaji kutokana na tafiti za kina na zenye kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya mifugo.

Alisema kwa sasa wizara iko katika mchakato wa kufanya mageuzi makubwa sekta ya mifugo na kuwa hilo litafanikiwa endapo kanda inayotoa mafunzo kwa wataalamu nao watafanya mageuzi katika ufundishaji.

Nzunda pia wametaka kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi, wakizingatia maadili na kwa bidii na uwajibikaji unaoz-

ingatia matokeo na usikivu kwa umma.

Alisema pia wanapaswa kujenga dhana ya ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi ili wawe sehemu ya maamuzi yanayofanya kwenye Idara na LITA kwa ujumla.

Kuhusu Baraza la Wafanyakazi la LITA, Nzunda alilitaka kuwa sehemu ya kutatua changamoto zinazokabili taasisi na wafanyakazi na si kuwa eneo la malalamiko na kuwalea watumishi wazembe na wasiotimiza wajibu wao.

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la LITA, Dk Pius Mwambene ambaye ni Mtendaji wa LITA alisema kutokana na juhudi mbalimbali za wizara kupitia LITA kumekuwa na ongezeko la udahili wa wanafunzi kutoka 2,536 hadi wanafunzi 3,972 katika kampasi nane.

Alisema pamoja na ongezeko la udahili la zaidi ya asilimia 50, kumejitokeza changamoto kadhaa zikiwamo za upungufu wa madarasa, upungufu wa wakufunzi hasa wa afya ya mifugo na uhandisi kilimo na kuomba wizara iwasaidie kupata basi ambalo litatumika kusafirisha wanafunzi wanapokwenda kwenye mafunzo kwa vitendo.

Alisema pia wakala imeanzisha utaratibu mpya wa kuwashikiza wanafunzi kwa wafugaji walio kwenye maeneo yao wakati wa likizo lengo ni kuwawezesha wanafunzi kujenga uzoefu na ujasiri wa kuwahudumia wafugaji mapema iwezekanavyo.

Kuhusu kikao hicho, Dk Mwambene alisema ni kupokea na kujadili mapato na matumizi ya wakala, kujadili mpango na kusimamia utekelezaji wake.